S. L. P. 1174
DODOMA, TANZANIA
Barua pepe: info@tastastat.or.tz
Mobile: +255 (0) 754757607
Tovuti: www.tastastat.or.tz

TAARIFA KWA WANACHAMA WOTE KUHUSU RATIBA YA MKUTANO MKUU WA NANE (8) WA CHAMA CHA WATAKWIMU TANZANIA – 2026

Ndugu wanachama wa Chama cha Watakwimu Tanzania (TASTA),

Kama ilivyotolewa taarifa kupitia tangazo la Chama la tarehe 27 Oktoba 2026, maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Nane (8) wa Chama yanaendelea vizuri. Mkutano huo umepangwa kufanyika kuanzia tarehe 13 hadi 16 Novemba 2026. Aidha, wanachama wote mnaalikwa kuhudhuria Siku ya Takwimu Afrika, inayoratibiwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa ushirikiano na TASTA. Pia, NBS imewasilisha mialiko kwa waajiri ili waruhusu watakwimu kushiriki maadhimisho haya.

Katika kuimarisha ushiriki wa wanachama, Chama kinapenda kuwafahamisha kuhusu ratiba ya shughuli mbalimbali zitakazofanyuka katika kipindi hicho kama inavyooneshwa hapa chini:

Na.	**Tarehe**	**Tukio**
1.	13 Novemba 2026	Mkutano Mkuu kwa kuzingatia ajenda zilizopangwa
2.	14 Novemba 2026	Uchaguzi wa viongozi wa TASTA
3.	15 – 17 Novemba 2026	Mafunzo na Mdahalo kwa watakwimu kuhusu Akili Unde (AI) na *Big-Data*
4.	18 Novemba 2026	Maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika

Wanachama wanakumbushwa wajibu wao wa kuhudhuria Mkutano Mkuu na kushiriki katika shughuli za Chama kwa mujibu wa Ibara ya 17 ya Katiba ya TASTA ya mwaka 2021 kwa maendeleo ya Chama na Taifa.

IMETOLEWA NA OFISI YA KATIBU

CHAMA CHA WATAKWIMU TANZANIA (TASTA)

8/11/2026